***Geuza Nguvu Yako ya Mauzo Kuwa Kipato Halisi na Godoro Point!***

## *TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI*

***Cheo**: **Afisa Magodoro***

***Mahali:*** Morogoro, Tanzania

***Idadi ya Nafasi:*** Mbili (**02), Wakazi wa Morogoro Mjini Tu**

***Aina ya Kazi:*** Kazi ya **Kudumu**

***Muda wa Kazi:*** **Saa 2:00 Asubuhi – Saa 2:00 Usiku, Siku 6 kwa Wiki**

***Malipo:*** Pata **Kipato kisicho na Kikomo** kupitia **Kamisheni ya Mauzo** yaliyofanikiwa!

## *MAELEZO YA KAZI (Job Description)*

**Afisa Magodoro** atahakikisha Mauzo yakiendelea, Wateja Kuridhika, na Duka kuwa Safi na lenye Mpangilio Mzuri kila Siku, huku akivutia Wateja Wapya kwa Weledi na Mbinu za Kisasa za Mauzo.

## *MAJUKUMU YA KAZI (Duties & Responsibilities)*

1. Kuwakaribisha na kuwahudumia Wateja kwa Ukarimu, Heshima na Weledi.
2. Kutoa Maelezo Sahihi na kuvutia kuhusu: - **Aina, Ubora, na Bei** za Magodoro na Bidhaa Nyingine.
3. Kusaidia Wateja kuchagua Bidhaa Bora kulingana na **Mahitaji** na **Bajeti** zao.
4. Kurekodi Mauzo kwa Usahihi na kutunza Kumbukumbu zote za **EFD** na Mauzo ya kila siku.
5. Kuhakikisha Duka linakuwa safi, limepangwa vizuri na Bidhaa zinaonekana kwa Mvuto.
6. Kusimamia **Hesabu Za Bidhaa *(Stock),*** Kupokea Bidhaa Mpya na Kutoa Taarifa za Upungufu Mapema.

7. Kufikia Malengo ya Mauzo kwa kutumia Ubunifu, Mbinu za Kisasa na Mitandao ya Kijamii kuvutia Wateja Wapya.
8. Kutekeleza Maagizo ya Viongozi kwa Uaminifu na kufanya kazi kwa Ushirikiano na Ari ya Mafanikio.

## *SIFA ZA MWOMBAJI (Qualifications & Requirements)*

1. Elimu ya Kidato cha Nne ***(Form IV)*** au **Zaidi**.
2. Uwezo Mzuri wa kuzungumza **Kiswahili Fasaha** na **Kiingereza.**
3. Uzoefu katika Mauzo, hasa Bidhaa za Nyumbani kama Magodoro au Samani (Uzoefu Utapewa Kipaumbele).
4. Ujuzi wa kutumia **Mashine za EFD** na kuandaa ***Risiti, Proforma Invoice, Tax Invoice, na Delivery Note***.
5. Ujuzi wa **Kompyuta** na Programu za ***Microsoft Office (Word, Excel, n.k.).***
6. **Simu Janja** inayofanya kazi vizuri na yenye Akaunti Hai za **Mitandao ya Kijamii.**
7. Uwezo wa kufanya kazi chini ya shinikizo na kufikia Malengo ya mauzo.
8. Umri kati ya Miaka **18** hadi **25.**
9. Uelewa wa Mazingira ya **Mkoa wa Morogoro** (atapewa kipaumbele).
10. Bidii, Uaminifu, na Utayari wa kufanya kazi kwa muda Mrefu na kwa Kujituma.

## *SIFA BINAFSI (Personal Attributes)*

1. Mchangamfu, Mwenye Nidhamu, na ana Uwezo wa Kushawishi na Kuhudumia Wateja.
2. Mkweli, Mwaminifu, na Mwenye Uwezo wa kufanya kazi bila Usimamizi wa karibu.
3. Mchapakazi, Mwajibikaji, na Mwenye Tabia Njema.
4. Mcheshi, Mkarimu, na Mwenye Tabia inayovutia Wateja.
5. Mwenye Ujasiri, Uvumilivu, na Kujiamini katika kuelezea Faida za Bidhaa.
6. Mbunifu na Mtumiaji wa Mitandao ya Kijamii kwa Ufanisi Kuvutia Wateja.
7. Ana Mwonekano Nadhifu unaojenga Imani na Heshima kwa Wateja.
8. Bidii, Ari ya Mafanikio, na Moyo wa kufanya kazi kwa Ushirikiano ***(Teamwork).***

## ***MAHITAJI YA KUOMBA KAZI***

Waombaji wanatakiwa kuwasilisha **Nyaraka zifuatazo kwa njia ya Kielektroniki *(Scanned Copies): -***

1. **Barua ya Maombi ya Kazi** – **Iandikwe Kwa Mkono**, ikiwa na **Anuani kamili na Mawasiliano sahihi** *(**Namba za Simu Na Barua Pepe**).*
2. **Wasifu Binafsi (Curriculum Vitae – CV)** – unaoonyesha **Taarifa zako Muhimu, Uzoefu wa Kazi**, na **Wadhamini Wawili (2)**.
3. **Nakala za Vyeti vya Elimu** – Vyeti vinavyohusiana na Sifa Zako.
4. **Nakala ya Vitambulisho halali *(NIDA, Leseni, au Kadi ya Mpiga Kura).***
5. **Picha Moja ya Pasipoti (Passport Size, Blue Background)**.

**KUMBUKA:** Hakikisha Nyaraka Zote ni za **Kielektroniki, Zilizosafishwa Vizuri**, ili Maombi Yako yashughulikiwe Haraka.

## ***JINSI YA KUOMBA***

Tuma Maombi Kwa: **godoropoint@yahoo.com**

Kichwa cha Habari**: *Afisa Magodoro – Maombi ya Kazi***

Anwani kwenye Barua ya Maombi:

Mkurugenzi Mtendaji
**GODORO POINT**
**39** Barabara ya Konga
S.L.P **649**
**67103** Morogoro, Tanzania

## ***TAARIFA MUHIMU***

1. **Godoro Point** ni Mwajiri anayetoa Fursa sawa kwa Wote bila Ubaguzi.
2. **Hakutakuwa na Posho wala Nauli** zitakazotolewa kabla ya Usaili.
3. **Ni Waombaji waliochaguliwa Pekee** watakaowasiliana nasi kwa ajili ya Usaili.
4. **Malipo yatatolewa tu baada ya Mauzo kufanikiwa Kikamilifu.**
5. **Mwisho wa kutuma Maombi:** Tarehe **10 Novemba, 2025.**

---

***Karibu ujiunge na Timu ya Godoro Point leo — Geuza Nguvu Yako ya Mauzo kuwa Kipato Halisi!***